

## **KANISA BORA HUANZIA NA MIMI**

Kuna mtu alisema “Kama unataka serikali njema, uwe raia mwema” Kwa kuzingatia hili, nami ningependa kupendekeza wazo hilo hilo kuhusiana na kanisa. Kama tunataka kanisa bora, mahali pa kuanzia ni kwetu wenyewe. Yesu alilifia kanisa ili liwe bora kadri iwezekavyo. Kwa mtazamo wa Uungu, kanisa ni kamilifu. Hata hivyo, kanisa haliko katika hali ipasayo katika maeneo mengi. Mara nyingi twaacha dhambi kutuingilia na kuzuia kanisa kuwa kama ipasavyo. Inapotokea hivyo, lazima tujue ya kuwa Siku ya Hukumu tutatakiwa kujibu! Hatuwezi kufanya jambo linaloharibu mwili wa Kristo ulio wa thamani alafu Mungu asione na kulipiza! Katika makala hii fupi, tutazingatia mambo fulani ambayo yatatumika kulifanya kanisa kuwa bora iwezekanavyo.

### **KAMA TUNATAKA KANISA LIWE BORA, LAZIMA TUTAMBUE KUWA SISI NI MUHIMU**

Tunatakiwa kuung’amua ukweli kwamba sisi ni muhimu bila kujali tuwezacho kufanya. Zingatia maneno ya Mtume Paulo kwa ndugu waliokuwa Korintho;

**Lakini sasa viungo ni vingi ila mwili ni mmoja, Na jicho haliwezi kuuambia mkono sina haja na wewe; wala tena kichwa hakiwezi kuiambia miguu, sina haja na ninyi. Bali zaidi sana vile viungo vya mwili vidhaniwavyo kuwa vinyonge zaidi vyahitajiwa zaidi. Na vile viungo vya mwili vidhaniwavyo kuwa havina heshima, viungo vile twavipa heshima zaidi, na viungo vile visivyo na uzuri vina uzuri zaidi. Kwa maana viungo vyetu vilivyo na uzuri havina uhitaji; bali Mungu ameuungamanisha mwili, na kukipa heshima zaidi kile kiungo kilichopungukiwa; ili kusiwe na faraka katika mwili, bali viungo vitunzane kila kiungo na mwenziwe. Na kiungo kimoja kikiumia, viungo vyote huumia nacho; na kiungo kimoja kikitukuzwa, viungo vyote hufurahi pamoja nacho (1 Wakorintho 12:20-26).**

Bwana anatutegemea tufanye lililo upande wetu kama inavyoonekana katika maneno ya Paulo kwa Waefeso (Waefeso 4:15, 16). Kila mmoja wetu ana sehemu katika kazi ya kanisa kama vile ambavyo kila kiungo cha mwili wa binadamu kinavyotenda kazi (1 Wakorintho 12:14-24). Bwana anatutegemea kulisaidia kanisa likue na kutenda kazi kama anavyotamani.

### **KAMA TUNATAKA KANISA LIWE BORA TULIFANYIE KITU FULANI**

Lazima tuwe wakarimu, wenye huruma, wasamehevu na walio tayari kusaidiana (Waefeso 4:31, 32; Wagalatia 6:1, 2). Sisi kama wakristo, tujifunze kutouliza nisaidie nini, bali lini naweza kufanya? Twaweza kulisaidia kanisa kukua kwa kuliinua badala ya kukosoa kinachofanywa ili likue, ali mradi kinachofanywa ni cha kweli katika Neno (1 Wakorintho 10:10. Sielewi kwa nini iko hivi, lakini ni kama wengine wapo kwa ajili ya kulalamika bila kujali uthubutu uliofanyika,. Imekuwa kama hurka kwamba kama ndugu hawalalamiki basi ujue hawajafurahi. Na hurka hii inatupelekea katika maisha duni yasiyo kifani. Namna mojawapo tunayoweza kufanya ili kulisaidia kanisa ni kuyachunga maisha yetu dhidi ya ya kutenda au kusema jambo ambalo litaleta fedheha kwa kanisa.

### **KAMA TUNATAKA KANISA LIWE BORA, LAZIMA TUWAALIKE WENGINE ILI WASHIRIKI BARAKA ZAKE**

Maisha ya kikristo ni maisha bora na yenye tunu ambayo mtu anaweza kuyaishi. Siyo tu tuamini kuwa hili ni kweli, bali pia tuishi kama ambavyo tunaamini. Mkristo amebarikiwa kimwili na kiroho (2 Wakorintho 9:6; Waefeso 1:3). Hakuna ukomo wa Baraka za Mungu awamiminiapo watoto wake waaminifu, isipokuwa tumejiwekea wenyewe ukomo (Luka 6:38; Wagalatia 6:7,8). Tunapomleta rafiki kwenye madarasa ya Biblia na ibada twamsaidia rafiki yule kuona kwamba Mungu amewabariki walio katika Kristo. Kanisa linalokua ni lile ambalo linaguswa na kuzipenda nafsi zinazopotea (Marko 10:21; Matendo 2:47).

Kanisa bora linaanzia na sisi wenyewe, na sasa ndiyo wakati wa kuanza.